# KISWAHILI KIDATO CHA TATU

# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

# KISWAHILI KARATASI YA TATU

# FASIHI 102/3

# MUHULA WA KWANZA

**MAJIBU-SHAIRI- SWALI LA KWANZA**

1.Mwerevu Hajinyoi(al1)

2.-Shairi hili lina beti tano

-Kila ubeti una mishororo minne-Tarbia

-Kila mshororo una migao miwili-ukwapi na utao

-Kila mshororo una mizani 16

-Vina vya nje vinabadilika ilhali vya ndani vinabadilika kutoka ubeti mmoja hadi mwingine.

-Mstari wa mwisho unarudiwarudiwa katika beti zote. (zozote 4x1=alama 4)

3.Utajiri /ukwasi –malenga anazungumzia mhusika mwenye mali.

- Majivuno/maringo-mwenye mali anaambiwa ana maringo kiasi cha kutotambua maovu anayoitendea jamii.

4.Jazanda-Neno kisu gutu limetumiwa kwa maana ya mtu mnyonge asiye na pato zuri.

5.-Matumizi ya lahaja-maivu,ndiya,kumvunda,mbiti n.k

-Inkisari-'meonekana, 'megenka

-Tabdila –akajinyowa,ujuwe,kahu,waliyo.

-Mazida-muwerevu.

-Kuboronga sarufi-wageukile badala ya wamegauka

6.Kutajirika kusikupumbaze ukajikiri kuwa una maarifa sana kwani kuringa kwako ndiko kutakuangamiza.

Wakati utafika,kutanabahi umekumbwa na hali ngumu usiyoweza kujinasua.

Hata mtu awe na maarifa au uwezo kiasi gani hajitoshelezi kwa kila kitu.

7.Kitu-mali/utajiri/ukwasi

Mtovu –maskini/mlala hoi/Hawinde.

Kusikughuri-kusikupumbaze/kusikundanganye.

## MAJIBU –SWALI LA PILI

- Mtemi Nasaba Bora alinyakua mali ya watu wa sokomoko.Anapogunduliwa anaamua kujiua.
- Mwalimu anajisifu kuchapisha mswada usiokuwa wake kwa jina lake.Anaungulika aliposhindwa kutoa mhadhara kuhusu uandishi wake katika chuo kikuu cha mkokotoni.
- Mtemi Nasaba Bora alikuwa karibu kuuawa na Oscar (Gaddafi)kwa sababu ya mauaji ya mamake na unyakuzi wa shamba lao.
- Kitoto uhuru kufa kutokana na kutowajibika kwa madktari.

- Wagonjwa wanakosa kuhudumiwa katika zahanati ya Nasaba bora.
- Oscar kambona alitiwa gerzani kwa kupatikana na furushi la bangi.
- Madhubuti anamkanya babake dhidi ya kumtafutia ajira kwa kutoa hongo.Mwishowe anahama kutoka katika kasri lao hadi kibandani.
- Ben Bella alitiwa gerezani kwa kukibaka kitoto
- Amani anaadhibiwa kinyama na mtemi Nasaba Bora na akumtupa kando ya mto kiberenge.
- Bi Zuhura anapewa talaka na mtemi Nasaba Bora kwa tuhuma za kushiriki mapenzi nje ya ndoa.
- Wasichana walipachikwa mimba nje ya ndoa.
- Mashaka kugeuka na kuwa mwehu baada ya Ben Bella kusitisha uhusiano wao wa kimapenzi
- Chwechwe makweche kuwa kiguru.
- Mtemi Nasaba Bora kupokea vitisho kutoka kwa lowela baada ya kuwafunga Amani na imani ambao hawakuwa na hatia.
- Viongozi walitoa idhini ya wafungwa kuteswa na pia hawakupewa chakula
- Serikali kutotilia maanani maslahi ya mashujaa ambao walikuwa wazalendo kindakindaki k.v Matuko weye,chwechwe makweche n.k
- Mtemi Nasaba Bora kushiriki mapenzi nje ya ndoa. (zozote 10x2=alama20)

**MAJIBU- SWALI LA TATU**

a)-Maelezo haya yanamrejelea mashaka,bintiye mtemi Nasaba Bora.

-Alikuwa amerejeshwa shuleni baada ya kujumuika na wazazi wake katika sherehe za siku kuu ya wazalendo.

-Alikuwa amepokezwa barua na mpenziwe Ben Bella mwanake Bwana maozi.

-Baada ya kupokea barua hiyo,mashaka aliingia msalani kisha kuisoma japo kidogo.

-Mashaka alipofikishwa shuleni jioni hiyo alikimbia moja kwa moja hadi kwenye chumba chake katika bweni,akajifungia ndani na kuanza kuisoma barua hiyo. (4x1=al4)

b)

- Ben Bella alimjulia hali mashakla
- Kuwa alipokuwa katika jela alijifunza kwamba bado hawajapata uhuru kamili
- Kuwa licha ya kufungwa jela,bado alimpenda mashaka.
- Alidhamiria kuwa ipo siku moja wangefunga ndoa na kuishi pamoja.
- Alikumbuka jinsi walivyokutana katika ukumbi wa mashindano ya densi.
- Hangeweza kutimiza ahadi yao ya ndoa kutokana na yale aliyoyapata nyumbani alipotoka jela.
- Babake mzazi alimpachika mimba lowela ambaye ni dadake kwa hivyo baba mkwe hawezi akawa shemejiye.
- Kuwa alielezwa na dadake kuwa ndiye aliyemzaa uhuru na akampeleka kisiri hadi mlangoni mwa Amani kwa mpango wake na mpenziwe,mtemi Nasaba Bora.

(zozote 4x2=alama8)

c)

- Mwandishi wa barua ni Ben Bella maozi.
- Ni msiri-Hawajulishi wazazi wake kuhusu uhusiano wa Lowela na mtemi Nasaba Bora.
- Ni mlanguzi wa dawa za kulevya-Ben Bella alikuwa lofa aliyekuwa na uraibu wa bangi.
- Mpenda raha-Alikuwa ashiki wa muziki wa kufokafoka .vilevile aliweza kunyakua taji la ubingwa wa kucheza disko katika jimbo zima.
- Ni mwenye msimamo thabiti-Anaamua kwa dhati kuvunja uhusiano wa kimapenzi na mashaka.
- Ni mbakaji-Alikuwa ametoka jela baada ya kuwa kule kwa miaka miwili kwa tuhuma ya kukibaka kitoto kidogo.

d) (zozote 4x1=alama4)

- Barua aliyopokea mwalimu majisifu kwenda kuitoa mhadhara Nchi ya wangwani.
- Barua ya madhubuti kwa babake Nasaba Bora akimjuvya kuwa anarejea nyumbani kutoka Urusi.
- Barua ya LOwela kwa mtemi Nasaba Bora.
- Barua ya madhubuti kwa Amani.
- Barua ya Amani kwa Imani.

(zozote 4x1=alama 4)

**MAJIBU-SWALI LA NNE**

Wizi/ufisadi-fimbo ya meya kuuzwa,

Kukatizwa kwa kandarasi ya mfanyabiashara

Mianya ya ufisadi katika ofisi ya meya.

I. Unyakuzi wa ardhi ya umma-meya amenyakua vipande vinne vya ardhi na mgawia Bili vingine.
II. Ubinafsi na tamaa-viongozi wana ubinafsi na tama iliyokithiri jambo linalochangia uongozi mbaya na kushiriki ufisadi.
III. Unafiki wa kidini-mhubiri analiombea baraza lidumu chini ya uongozi wa mstahiki meya na anajua shida zinazowakumba wanacheneo.
IV. Migomo-insababisha kuzorota kwa miundo ya misingi yote ya baraza la cheneo k.v usafiri,usafi wa baraza,huduma za afya n.k
V. Utabaka-matajiri wanaishi maisha ya kifahari k.v meya ilhalib wanacheneo wengine wanaishi maisha ya kubahatisha.
VI. Mapendeleo/ukabila-mhazili alipewa kazi na meya kazi ambayo akulingana na meya hakustahili kuipata.
VII. Ushauri mbaya-Bili,Diwani I na Diwani II
VIII. Wanampa meya ushauri wa kupotosha jambo linalowasukuma wanacheneo katika lindi la umaskini.
IX. Mauaji-waandamanaji wanashambuliwa kwa rungu,bunduki,vitoa machozi na magari yanayotapika maji.

X. Ubadhilifu/ufujaji wa hela za baraza-meya kumpeleka bibiye ulaya akajifungulie huko,kumpeleka Bili kwenye hoteli ya kujifahari ili wakajivinjari.
XI. Uongozi wa kiimla/udikteta-meya anatumia mabavu kuliongeza baraza na wanacheneo.
XII. Uongo/matumizi ya propaganda-meya anapondanganya kuwa dawa zimeagizwa pia wananchi wanapewa ahadi zisizoweza kutimilika.
XIII. Upyaro wa viongozi –Dida analalamika kutoheshimiwa,kutusiwa na kudhalilishwa na meya.

(zozote 10x2=alama 20)

**MAJIBU –SWALI LA TANO**

5a)

- Maneno ya mhubiri
- Anamwambia mstahiki meya
- Walikuwa katika ofisi ya meya wakati wa adhuhuri
- Alisema maneno haya kujibu ombi la meya la kumtaka amsamehe kwa sababu Gedi na askari wawili waliingia ndani na kuwashtua walipokuwa wakiendelea na maombi.

b) (4x1=alama4)

Mzungumzaji ni mhubiri

- Ni mnafiki-Analitumia jina la mwenyezi mungu na Dini kwa njia mbaya
- Mcha mungu-Anashughulikia suala la maombi katika baraza.
- Mwenye ubinafsi-Anajali maslahi yake kuliko ya wengi,Anapongeza uingozi mbaya wa meya ili aendelee kunufaika.
- Ni mwoga-wanapoamriwa walale,anayatimiza haraka bila pingamizi.
- Ni mwenye imani hafifu-Anaamini kuwa maombi yake yamejibiwa wakati Gedi na Askari wanapoingia na kuamuru wapige magoti.
- Ni mwenye kuwajibika-Anatimiza ahadi ya kifika katika ofisi ya meya na kumwombea.

(zozote 6x1=alama 6 )

c)

- Mgogoro baina ya meya na wanacheneo
- Mgogoro wa nyongeza ya mishahara

- Migogoro ya ardhi
- Migogoro baina ya wafanyakazi na wafadhili.
- Mgogoro baina ya meya na wawakilishi wa wafanyakazi.
- Mgogoro baina ya meya na wafadhili
- Mgogoro baina ya meya na Diwani III na siki(migogoro ya kimaoni)
- Migogoro baina ya watawala na watawaliwa

(zozote 5x2=alama10)

Manafunzi afafanue hoja ili kupata alama zote.

**MAJIBU –SWALI LA SITA**

I. Dereva mzungu kukataa kumbeba fikirini katika kituo rasmi cha magari.
II. Polisi wazungu kuwatoza waafrika faini kwa kuvuka barabara huku taa za kuelekeza magari zikiwaka ilhali wazungu hawatozwi.
III. Wanafunzi wazungu chuoni kupewa alama za juu ilhali waafrika alama za chini.
IV. Madukani mwafrika huandamwa na kushukiwa kuwa mwizi.
V. Magereza yameundiwa watu weusi.
VI. Wamerikani weusi wandhulumu waafrika weusi wenzao.
VII. Fikirini kushtakiwa kwa kutofunga zipu.
VIII. Wazungu kuwa na kasumba kuwa Afrika kumejaa uchawi.
IX. Hotelini,weusi hutazamwa kwa dharau na wateja na wahudumu.
X. Kuulizwa maswali ya dharau na wahadhiri wazungu na wanafunzi weupe.
XI. Kasumba kuwa Afrika kuna magonjwa ya kila aina.

(zozote 10x2=alama20)

**MAJIBU –SWALI LA SABA**

7a)

- Mawazo yanayompitia Fikirini akilini mwake.
- Yuko katika nyumba ya Fiona na Bob.
- Ni wakati ambapo Fiona na Bob wanataka kumwua Fikirini.
- Hii ni baada ya kumvua nguo na kugundua kwamba hana pesa zozote.

b) (zote4x1=alama4)

- Takriri/urudiaji-siku ya siku
- Methali –siku ya nyani kufa miti yote huteleza

(zote2x2=alama4)

b)Maudhui

- Ubaguzi wa rangi-Dereva kumwacha kwa sababu ni mweusi.

- Elimu –Fikirini ameenda marekani kupata Elimu ya juu.
- Uozo wa jamii-Fiona kutaka kushiriki ngono na fikirini kwa malipo
- Ukatili /Dhuluma-Bob na Fiona kumvua Fikirini nguo,kumwibia,kutaka kumuua.
- Unyanyasaji-wazungu kuwanyanyasa watu weusi

  Fikirini kutuzwa maki ndogo katika mitihani

  Kuhukumiwa kwa kutofunga zipu ya suruali

- Tamaa –Fiona na Bob wana tamaa ya pesa
- Kasumba ya wazungu-kujiona bora kuliko watu weusi,kumwuliza Fikirini maswali ya kijinga kuhusu Afrika na waafrika.

**MAJIBU SWALI LA NANE**

8a)Misimu ni semi zinazozuka miongoni mwa makundi maalum ya watu na kutumika kwa muda mfupi kasha kutoweka kuibuka ingine.(alama2)

b)Visasili ni ngano zinazosimulia asili/chanzo cha matukio katika jamii.

Visakale ni masimulizi ya kimapokeo ya matukio yaliyotendeka zamani au kale. (2x2=alama4)

c)

- Hueleza kuhusu majagina /mashujaa
- Chuku hutumiwa katika utambaji wake
- Matumizi ya nyimbo
- Huwa na ukweli wa kihistoria
- Husimulia mambo ya kiajabu
- Majagina huwa na siri ya nguvu na uwezo wao
- Majagina huzuka kutokana na migogoro katika jamii.
- Mashujaa hupigania wanyonge katika jamii
- Baadhi ya mashujaa huwa na maumbile ya ajabu. (zozote 4x1=alama4)

d)Huelimisha

Huburudisha

Hufuunza maadili

Hurithisha utamaduni kutoka kizazi hadi kizazi

Huhifadhi historia na utamaduni wa jamii

Huimarisha umoja/ushirikiano wa wanajamii

Huonya na kutahadharisha

Kitambulisho cha jamii. (zozote 5x1=alama5)

b)

- Ukosefu wa utafiti madhubuti
- Ukosefu wa walimu wa kutosha wa somo hili
- Uhaba wa vitabu vya kurejelea
- Fasihi andishi kuzingatiwa mno
- Baadhi ya vipera ni kinyume cha maadili ya kidini.
- Vijana wa sasa hawaonei fasihi hii fahari
- Mtazamo hasi kuwa haina manufaa ya kuelimisha watu. (zozote 5x1=alama5)